HakiElimu
Education Brief No.07.3K


# Fedha za Elimu zinatumiwaje?

## Uchanganuzi wa Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi[i]


*Bajeti ni kuhusu kufanya chaguo kipi cha kukipa kipaumbele na kipi cha kukiacha. Maelezo haya yanachunguza matumizi ya Wizara inayowajibika kwenye elimu mwaka 2005/06. Pia, inalinganisha matumizi halisi dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, na upangaji wa muda muafaka ambapo fedha zilitumika.*

### Mambo Gani huunda Bajeti ya Elimu?

Hotuba za bajeti husisitiza vipaumbele, lakini mara nyingi huacha maelezo ya kina. Mtazamo wa karibu wa tarakimu za bajeti kwa undani, kwa mwaka 2005/06 unaonesha kwamba vipaumbele vilivyowekwa mwanzoni mwa mwaka kwa ajili wizara ya Elimu vilikuwa mishahara, gharama za shule, na gharama za uendeshaji.




Matumizi halisi ya fedha yalikuwaje? Uchunguzi unaonesha kwamba kulikuwa na tofauti kubwa kati ya bajeti iliyopitishwa na Bunge na jinsi ilivyotumiwa na wizara.




Wakati ambapo bajeti iliyopitishwa ilikuwa shilingi bilioni 178, matumizi halisi yalikuwa shilingi bilioni 103 tu, au kiasi cha 58% ya jumla. Mishahara na gharama za shule viliendelea kuwa vipaumbele lakini masurufu, mikutano, ukarimu na safari pia vilipewa kipaumbele, vikichukua sehemu kubwa zaidi ya bajeti.

### Tofauti kuu zilikuwa zipi?

Fedha nyingi zilizoidhinishwa na Bunge, zinazofikia shilingi bilioni 75, hazikutumika. Mtazamo wa karibu wa data unaonesha :

- Shilingi bilioni 14.6 ziliidhinishwa kwa ajili ya ruzuku maalumu kwa kila Mwanafunzi lakini hakuna fedha zilizotengwa au kutumika
- Shilingi bilioni 12.4 ziliidhinishwa kwa ajili ya "Shule" lakini hakuna fedha zilizotengwa au kutumika
- Pungufu ya nusu ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya chakula cha shule zilitumika.

**Matumizi 10 ya chini kwa maelezo ya utondoti**

| Maelezo ya Akaunti | Salio la Bajeti (Mabilioni ya Shs.) | Salio la Bajeti (% ya Bajeti) |
|---|---|---|
| 1. Ruzuku maalumu ya SEDP kwa kila mwanafunzi | 14.6 | 100% |
| 2. Kiasasi | 13.5 | 97% |
| 3. Shule | 12.4 | 100% |
| 4. Ada | 6.0 | 59% |
| 5. Chakula cha Shule | 4.6 | 45% |
| 6. Vifaa | 4.3 | 94% |
| 7. Majengo | 3.3 | 70% |
| 8. Vifaa vya Mafunzo | 3.0 | 58% |
| 9. Uchapaji | 2.4 | 90% |
| 10. Ugavi wa Vifaa vya Kuandikia | 2.1 | 67% |


Vitu vichache vilinunuliwa kutokana na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Uchunguzi wa karibu zaidi wa maeneo matano ya juu ya kutumia zaidi ya kiwango unadhihirisha aina za shughuli zilizoonekana kupewa kipaumbele. Muhimu zaidi, matumizi ya bajeti ya chakula yalizidi kwa zaidi ya shilingi bilioni moja. Hili linashangaza sana kwa kuzingatia kwamba pungufu ya nusu ya kiasi

| Matumizi 5 yaliyozidi, kwa maelezo ya utondoti | | |
|---|---|---|
| Maelezo ya Akaunti | Salio la Bajeti (Mamilioni ya Shs.) | Salio la Bajeti (% ya Bajeti) |
| 1. Chakula | (515.0) | 132% |
| 2. Huduma na matengenezo | (138.7) | 47% |
| 3. Kazi za ziada | (2.9) | 0.5% |
| 4. Safari za Likizo | (2.7) | 1.1% |
| 5. Ofisi | (2.2) | N/A |

kilichoidhinishwa kilitumika kwenye chakula cha shule. Maeneo mengine yaliyovuka matumizi ni pamoja na masurufu, ofisi, huduma na ukarabati, vitu vyote ambavyo vinaweza kujengewa hoja kwamba si vipaumbele kwa kuboresha elimu kwenye ngazi ya jamii.

**Vipi Kuhusu Wakati muafaka wa Kutumia?**

Suala la pesa zinatumika wakati gani pia ni muhimu katika kuamua ubora wa matumizi, kwa vile utoaji uliochelewa unaweza kuvuruga mipango na kusababisha matatizo makubwa katika ngazi ya shule. Wakati wengine wanahitaji kulipwa kwa mujibu wa utaratibu wa '1/12' (yaani uwiano wa jumla ya bajeti yote kila mwezi) wakati mwingine wengine wanataka kulipwa kwa mkupuo. Wakati hili linaeleweka, Wizara ya Elimu inaelekea ilitumia kiasi kikubwa katika mwezi wa mwisho wa mwaka wa fedha.




Kwa ujumla, katika mwaka 2005/06, 18% ya bajeti yote ilitumika katika mwezi wa mwisho, ikimaanisha zaidi ya 1/12, au 8.3% ya matumizi yote. Ni bayana kwamba, wakati matumizi ya mishahara yamekuwa thabiti na katika muda muafaka matumizi kwenye vitu kama magari (63%), ukarimu (52%), masurufu (38%) na safari (37%) yametokea kwa kiasi kikubwa, katika mwezi wa mwisho wa mwaka.

**Wizara ya Elimu Inapaswa Kufanya Nini?**

Elimu ni kipaumbele dhahiri katika bajeti ya 2007/08, na Wizara ya Elimu iko tayari kupokea fedha zaidi. Hata hivyo, uchambuzi wa 2005/06 unadhihirisha kwamba Wizara hiyo inaona vigumu kubajeti kwa elimu bora, na kusimamia matumizi halisi. Hususan, Wizara inahitaji:

- Kuandaa bajeti inayotoa vipaumbele bora kwa mambo yatakayoboresha ubora wa elimu kwenye kiwango cha shule.
- Kuhakikisha matumizi yake halisi yanalandana na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Hususan, ilipie kikamilifu mambo kama vile ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi ambavyo vinaweza kuboresha mazingira ya kujifunzia shuleni kwa kiasi kikubwa.
- Kupunguza bajeti matumizi ya vitu vinavyozidi viwango vya matumizi ambavyo si muhimu kwa ngazi ya shule. Kama vile chakula na masurufu kwa wafanyakazi wa Wizara.
- Kuongeza uwazi wa bajeti katika matumizi halisi kwa kutoa taarifa hii kwenye tovuti ya wizara ya elimu, katika ofisi za wilaya na maktaba za umma nchini kote.

---

[i] *Zingatia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inawajibika kwa pungufu ya nusu ya jumla ya matumizi ya elimu, kwa vile kiasi kikubwa cha fedha za elimu ya msingi kinapitia Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Taarifa zote zilizotumika katika maelezo haya zinatokana na 2007 Public Expenditure and Financial Accountability Review (PEFAR), ambayo yanaratibiwa na Benki ya Dunia.*

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu (255 22) 2151852/3 • Faksi (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org